

Kuibuliwa kwa Vipimo vya Umaskini vilivyofichika: Mtazamo wa Tanzania Bara



Kazi ya utafiti katika
Mikoa mitano Tanzania Bara

“Nchi yetu ina maadui watatu wakubwa. Umaskini, maradhi na ujinga”.

Mwalimu J.K. Nyerere, rais wa kwanza wa Jamhuri ya Muungno wa Tanzania, kauli aliyoitoa miaka ya mwanzo ya uhuru wa Tanganyika (Tanzania Bara).

“Kazi hii kwa unyenyekevu mkuu tunaitolea wakfu kwa watu wote wa Dunia ya Nne walotengwa na Dunia hii”

Yaliyomo

SHUKRANI.....	1
UTANGULIZI.....	2
MBINU ZA UTAFITI	3
KUSUDI LA LENGO KUU LA UTAFITI	4
UUNGANISHAJI MAARIFA	5
MATOKEO YA UTAFITI.....	6
VIPIMO VYA ASILI.....	8
1. Elimu Duni	9
2. Afya Mbovu.....	12
3. Umaskini wa Kipato	15
VIPIMO VYA UMASKINI VILIVYOFICHIIKA	
KUTOKA KATIKA MIKOA MITANO YA TANZANIA	18
1. Mazingira na Makazi duni	19
2. Ushirikiano wa watu wanaoishi katika umaskini	22
3. Ukatili, Unyanyasaji na ukandamizaji dhidi ya wanawake na watoto	24
4. Mmomonyoko wa maadili	27
5. Mila na Desturi	30
6. Mapungufu katika utekelezaji wa sera za taasisi.....	33
7. Kilimo kisichokuwa na tija	37
8. Unyanyasaji na kutengwa na jamii	39
9. Ulinzi na malezi duni ya wazazi na jamii	41
10. Athari za kisaikolojia zinazosababishwa na Umaskini	43
HITIMISHO NA MAPENDEKEZO.....	46
TIMU YA UTAFITI YA ATD TANZANIA	50
VIAMBATANISHO	51

SHUKRANI

Sisi timu ya utafiti Tanzania bara tunatoa shukrani kwa waliobuni, kuwezesha na kusababisha utafiti huu ufanyike hapa Tanzania Bara.

Tunatoa shukrani za dhati kwa wanaharakati wote ambao walitoa muda wao adhimu na kuchangia katika utafiti huu. Bila maarifa yao na uzoefu wao wa umaskini uliokithiri kazi hii isingefanikiwa.

Shukrani kwa wanataaluma na wataalamu ambao walitoa muda wao **katika** utafiti huu. Mchango wao mkubwa umeifanya ripoti hii kuwa kama ilivyo. Muda wao walioutoa kwa kufanya kazi pamoja na makundi rika mengine ulikuwa na thamani sana kuwafanya watafiti wawe kama walivyo leo.

Shukrani kwa mamlaka na taasisi ambazo zilishrikiana kwa karibu na timu ya utafiti na hivyo kuiwezesha timu kufanya utafiti hadi hitimisho lake. Timu pia tunatoa shukrani zetu kwa wakosoaji wote ambao walichukua muda wao kukosoa baadhi ya maeneo katika ripoti hii. Mchango wa NBS unatambuliwa.

Wote wale waliosaidia kufikia uelewa bora wa umaskini Tanzania bara tunawashukuru kwa dhati.

Asante sana.

UTANGULIZI

Timu ya mradi wa Utafiti (ATD) ilifanya mradi wa utafiti wa miaka mitatu kuanzia mwaka 2016 hadi 2019, kubaini vipimo vipyta vya umaskini kwa lengo la kuibua “Mtazamo Mpya wa Umaskini” Tanzania Bara. Mradi huu ulikuwa wa kwanza katika kutafuta majibu mapya ili kuelewa umaskini ni nini na vipimo vyake. Lengo kuu la utafiti lilikuwa kubainisha vipimo vya umaskini ambavyo ni muhimu katika maisha ya watu na kuelewa mahusiano mionganoni mwa vipimo hivyo. Muktadha ulikuwa malengo endelevu ya Umoja wa Mataifa katika nia ya “kumaliza umaskini kila mahali katika namna zake zote ” (Lengo 1) na “hadi kufikia mwaka 2030, kupunguza angalau nusu ya idadi ya wanaume, wanawake na watoto katika umri wowote wanaoishi katika umaskini katika vipimo vyake vyote kwa kuzingatia ufanuzi wa kitaifa”. (Lengo 1.2). Pia mradi huu wa utafiti unakwenda sambamba na mkakati wa kitaifa wa kupunguza umaskini (MKUKUTA II). Unalenga kutumia ushahidi na matokeo ya utafiti kwa ajili ya kuboresha ufanisi wa utungaji wa sera na utekelezaji wake, kwa faida ya watu maskini wanaoishi vijijini na mijini. Lengo hili la utafiti liliwahamasisha timu ya mradi wa utafiti (ATD) kuwafikia makundi mengi ya watu wenye umri tofauti kadri inavyowezekana (watu wazima, wazee, vijana na watoto) wenye uzoefu wa moja kwa moja wa umaskini, pamoja na wataalamu na wanataalamu, kwa kutumia mbinu mpya shirikishi yaani “Uunganishaji Maarifa”. Matokeo ya utafiti huu ni ufanuzi wa dhana mpya ya umaskini na vipimo vyake.

Vipimo hivi vipyta vitawasaidia watungasera kushughulikia matatizo sahihi, kubuni programu zinazofaa, na kuelewa iwapo wanaleta mabadiliko. Utafiti huu ulikuwa ni sehemu ya utafiti wa kimataifa ambao ulitekelezwa katika nchi nyingine tano (Bangladesh, Bolivia, Ufaransa, Uingereza na Marekani) na uliratibiwa na makao makuu ya ATD yaliyo Paris, kwa kushirikiana na watafiti kutoka chuo kikuu cha Oxford Uingereza. Tanzania Bara, utafiti ulifanyika mjini na vijijini katika mikoa mitano, ambayo ni Dar es salaam, Dodoma, Kilimanjaro, Njombe na Kigoma.

Taarifa hii inaonesha vipimo vya umaskini vilivyokuwa vimefichika ambavyo vinafanuliwa na kuelezeza, kwa ajili ya kuunda uelewa mpana wa mtazamo mpya wa umaskini Tanzania Bara.

Mbinu ya utafiti

Utafiti huu kwa mara ya kwanza ulitumia mbinu pekee shirikishi iitwayo “Kuunganisha Maarifa” ili kutambua vipimo vyta umaskini vilivyofichika ambavyo vina athari kubwa katika maisha ya watu. Mbinu hii imejipambanua yenye na mbinu nyingine zilizo-zoeleka kama mbinu imara, ikihusisha sauti za wale “wasio na sauti” katika kuzalisha maarifa, hususani katika masuala yanayohusiana na maisha ya watu na ustawi wao. Hii inajionesha katika matokeo na data zilizowakilishwa katika ripoti hii.

Kupitia mbinu ya “Kuunganisha maarifa”, watu wanaoishi katika umaskini uliokithiri na kutengwa na jamii wanawezeshwa kubadilishana mawazo na kupeana maarifa na makundi mengine ya watu wasioishi katika umaskini, kama vile wanataluma, wataalamu, watungasera, wanahabari, na watu wengine kutoka katika jamii bila kujali asili yao na nafasi yao katika jamii. Kwa njia hiyo watu wanaoishi katika umaskini wanahuishwa kama watafiti-wenza, na wazalishi-wenza wa maarifa, kama yalivyo makundi rika mengine. Lengo ni kuondoa tofauti katika uzoefu wa kimaisha, katika kuzungumza, na kuffkiri, ili kuwezesha majadiliano yenye tija. Maarifa yaliyotokana na makundi haya yaliunganishwa pamoja kuleta uelewa na makubaliano ya pamoja kuhusiana na umaskini na vipimo vyake. Timu ya Mradi wa Utafiti (ATD) ilitaka kuhakikisha kwamba utafiti huu hauwangili wala hauwatumii wale wanaoishi katika umaskini uliokithiri.

Kusudi na lengo kuu la utafiti

Lengo kuu la utafiti lilikuwa ni kutambua vipimo vya umaskini ambavyo ni muhimu katika maisha ya watu na kuelewa mahusiano mionganoni mwa vipimo hivyo. Muktadha uliotumika ni ule wa Malengo Endelevu ya Umoja wa Mataifa na utashi wa kukomesha “umaskini katika aina zake zote kila mahali” (Lengo 1) na “kupunguza idadi ya wanaume, wanawake na watoto wa rika zote wanaoishi katika umaskini kufikia nusu yake ifikapo mwaka 2030 katika vipimo vyake vyote kulingana na ufanuzi wa kitaifa” (Lengo 1.2). Mradi huu vile vile unakwenda sambamba na mkakati wa kitaifa wa kupunguza umaskini katika nia yake ya kutumia ushahidi wa matokeo ya utafiti katika kuongeza ubora wa malengo na utekelezaji wa utungaji wa sera kwa faida ya watu wanaoishi katika umaskini katika ngazi za vijiji na mijini.

Mradi unatarajia kuwezesha na kuinua ufikiri wa kimataifa kuhusiana na asili ya kupima vipimo vya umaskini kwa kushirikisha sera ya jumuiya ya kimataifa pamoja na uzoefu na uelewa, mantiki za walio na uzoefu wa maisha ya umaskini uliokithiri katika tamaduni zao na aina za maendeleo yao. Kwa kutoa kipaumbele kwa maarifa ya wanaoishi katika umaskini na kuunganisha na ufahamu wa kisayansi pamoja na mitazamo ya wataalamu na umma wote, utafiti kwa namna ya pekee utaweza kufikia mitazamo ya pamoja katika:

1.

**Vipimo vya umaskini:
Umuhimu wake na mahusiano
katika miktadha mbalimbali na
viwango vya sifa zake na
mahusiano mionganoni mwake**

2.

**Matokeo haya yanamaanisha nini
katika ufahamu uliopo kuhusiana na
umaskini na vipimo vyake,
maendeleo katika sera na mapokeo
yake kulingana na vipimo na
viashiria vya umaskini kitaifa.**

Zaidi ya hayo, mradi unalenga kuleta matokeo bora ya uwezeshaji na kufikiri mipaka ya kijamii na kielimu kwa washiriki wote, kutoa mafunzo kwa watu walio na uzoefu wa umaskini na kutathmini michakato inayotokana na ushirikishwaji huu na hivyo kuweza kutumika katika tafiti zingine.

Uunganishaji Maarifa

Maana ya Uunganishaji Maarifa

Utafiti ulitumia kanuni na namna ya utafiti uliopewa jina la “Uunganishaji Maarifa” kwa kuwashirikisha watu walio na uzoefu wa moja kwa moja wa umaskini kama njia ya kufikia lengo la utafiti. “Uunganishaji Maarifa” ni mchakato ambao kupitia kwake maarifa yanatambuliwa na kuwekwa pamoja kisha kuchambuliwa na kutengenezwa kwa umakini kwa mchakato wa kidemokrasia ndani ya vikundi vidogo vidogo (Fourth World-University Research Group, 2007). Utafiti huu unaweza kutofautishwa na tafiti nyingine kwa namna yake ya uhuru wa kujieleza katika mijadala inayoruhusu mabishano na hatimaye makubaliano ambayo hutokana pia na mahusiano ya kuaminiana mionganoni mwa wote wanaohusika katika kukusanya habari na maarifa yanayozalishwa.

Utaratibu wa “Uunganishaji Maarifa”

Baada ya wale ambao wana uzoefu wa umaskini pamoja na wale wasio na uzoefu (Wanataluma na wataalamu) kufikiwa, kupatikana na kuratibiwa katika vikundi rika, mchakato wa uunganishaji maarifa ulihuisha hatua zifuatazo:

Hatua ya 1:

Kila mshiriki katika kikundi rika alitakiwa kubainisha sifa, sababu (visababishi) na athari za umaskini ambazo zinajulikana kwa ujumla wake ndiyo masuala mbali mbali yanayohusiana na umaskini, yaani masuala yale anayofikiria kwamba ni ya muhimu.

Hatua ya 2:

Kila mmoja katika kikundi rika alishirikishana mawazo yake na wenzake baada ya hapo walitengeneza orodha moja ya masuala ya umaskini. Walijadiliana kwa kina na baada ya majadiliano ya pamoja orodha hii iliwekwa katika makundi kufuatana na masuala yaliyokuwa na maana sawa au yaliyokuwa yanafanana au yale yaliyokuwa na uhusiano wa karibu baadaye yalipewa majina ambayo ndiyo majina ya vipimo.

Hatua ya 3:

Vikundi rika kutoka wilaya moja vilikutana kwa muda wa siku mbili au tatu kuunganisha vipimo ili kupata vipimo vya vijijini na mjini katika ngazi ya wilaya.

Hatua ya 4:

Wawakilishi kutoka vikundi rika vya wilaya moja ya vijijini na ingine ya mjini vilikutana kuunganisha vipimo vya vijijini na mjini vilivyokuwa na uhusiano wa karibu kupata vipimo vya mkoaa.

Hatua 5:

Timu ya ATD ya utafiti iliunganisha vipimo vilivyokuwa na uhusiano wa karibu kutengeneza vipimo vya mikoa mitano iliyokuwa imechaguliwa kwa ajili ya utafiti.


MATOKEO YA UTAFITI

Sura hii inaelezea matokeo ya utafiti wa kitaalamu uliofanyika katika mikoa mitano iliyochaguliwa kutoka Tanzania Bara kuanzia mwaka 2016 hadi 2019 ukihusisha watu wazima kuanzia miaka 18 hadi miaka 60, wazee walio zaidi ya miaka 60 na watoto kati ya miaka 9 hadi 16 ambao wote walikuwa na uzoefu wa maisha ya umaskini, pamoja na wataalamu na wanataaluma. Katika utafiti huu maarifa yalikusanya kutoka katika vikundi rika lengwa vya vijiji ni vya mijini. Utafiti huu ulionesha tofauti ya mitazamo na uelewa wa umaskini ambao ni zaidi ya vipimo vya asili (umaskini wa kipato, elimu na afya duni). Maarifa haya mapya yalitengeneza vipimo vingine vilivyokuwa vimejificha. Vipimo hivyo ni vya kimaumbile, kijamii, kiuchumi, kisiasa na kisaikolojia/kiroho na vina matokeo hasi katika maisha ya watu, hususani wale wanaoishi katika umaskini, na mara nyingi haviwekewi maanani.

Vipimo vya Umaskini

Hatimaye jumla ya vipimo 67 viliibuliwa kutoka katika jumla ya vikundi rika 45 vikijumuisha watu wenyewe uzoefu wa moja kwa moja wa umaskini na wengine, yaani wataalamu na wanataaluma kutoka katika mikoa mitano iliyokuwa imechaguliwa kwa ajili ya utafiti. Vipimo hivi viliibuliwa na vikundi rika vya watu mbalimbali kama vile ; watu wazima kati ya umri wa miaka 18 hadi 60, wazee walio zaidi ya miaka 60, wataalamu na wanataaluma, vijana wenyewe umri zaidi ya miaka 16 chini ya miaka 18 na watoto kati ya umri wa miaka 9 na 16. Vipimo vilipitiwa na kuunganishwa na timu ya utafiti hatua kwa hatua. Mkakati wa kuunganisha vipimo ultoa jumla ya vipimo 10 vya umaskini vilivyofichika na vipimo vitatu vya asili yaani Umaskini wa Kipato, Elimu duni na Afya mbovu hivyo kufanya jumla ya vipimo 13 vya umaskini vinavyotoa maana na uelewa wa asili ya umaskini unaoathiri watu wa Tanzania bara.

Mchakato wa kuunganisha maarifa kupata vipimo vya mikoa
mitano iliyochaguliwa kutoka Tanzania Bara



Vipimo vya Asili



Hivi ni vipimo vinavyojulikana ambavyo vinasababisha madhara katika maisha ya watu, hususani wale walio katika uzoefu wa moja kwa moja wa umaskini. Licha ya juhudi zote ambazo zimekuwa zinafanywa na serikali kushughurikia vipimo hivi bado vinachukuliwa kwamba ndivyo chanzo kikuu cha umaskini na vinaathiri watu wengi nchini kote ; watu ambao ni maskini hudidimia katika umaskini zaidi.

01. Elimu duni



Maana: Kipimo hiki kinahusu aina ya elimu ambayo haitoi ujuzi na maarifa ya kuwawezesha watu kuwa wabunifu na kujitegemea katika mapambano dhidi ya umaskini.

Maelezo ya kipimo

Suala la maendeleo linapopewa kipaumbele, suala la elimu ni la kipekee kabisa. Kuna usemi unasema “Elimu ni msingi wa maendeleo” kwa kizazi chochote kile. Inapokuja katika suala la mapambano dhidi ya umaskini, elimu inakuwa ni suala la msingi hususani kwa vijana, watu wazima na wazee wanaoishi katika umaskini. Licha ya kuongezea uwezekano wa kupata ajira, (na hivyo kupunguza fursa za kuteseka kutokana na umaskini wa kipato) elimu ina athari katika nyanja za maisha, kwa mfano kujua kusoma, kuandika ni ujuzi unaotumika katika shughuri nyingi za kila siku kama vile kufanya biashara. Miongoni mwa madhara mengine wanayokabiliana nayo, watu wasiojua kusoma na kuandika ni kutengwa katika jamii na kuwa na wakati mgumu katika kupata habari. Ukoefu wa elimu bora unaweza kumsababishia mtu kuwa na matarajio finyu sana katika maisha, kutojiamini na kutojali sheria. Hii inaweza kusababishwa na sababu nyingi kama vile kutokutambua na kutokutumia maarifa na ujuzi wa asili, kutokuwepo mazingira wezeshi kwa ajili ya ubunifu, kukosa walimu wenye ujuzi, ongezeko la watoto wanaoacha shule, vifaa vya kujifunzia visivyotosheleza, maadili, mila na desturi mbovu katika jamii na umaskini. Kukosa vifaa kwa ajili ya mafunzo ya ufundi stadi ili kuweza kujifunza ujuzi pia ni suala linalochangia. Hali ni mbaya zaidi katika maeneo ya vijijini ambako wazee wengi hawajui kusoma na kuandika.

Watu wenye uzoefu wa moja wa moja na umaskini wasio na uwezo wa kujigharamia kupata elimu bora wanaathirika zaidi kutokana na uelewa wao mdogo katika masuala muhimu kama vile uzazi wa mpango, ufahamu wa kisayansi katika kuboresha kilimo na uwezo wa kutawala rasilimali. Wanateseka kutokana na kukosa ujuzi wa ujasiriamali, kutoweza kutumia uwezo binafsi na kiwango cha juu cha kutojua kusoma na kuandika. Haya yote huwasababisha kuwa maskini zaidi.

i. “Binti yangu nakuomba, tafadhali usifanye vizuri katika mitihani yako. Ni vema ushindwe mitihani yako kwa sababu sina uwezo wa kukulipia ada na pia ninaogopa kuadhibiwa na serikali nisipokupeleka shule ukishinda mitihani yako’. Niliposikia maneno ya mama yangu, nilitekeleza kama alivyoniomba ili kumridhisha. Sikujua kama siku moja nitajutia uamuzi huo. Kweli, sasa naujutia sana uamuzi huo. Ningefanya vizuri mitihani yangu ningeweza kuendelea hadi chuo kwa sababu nilikuwa na akili sana darasani”

(Mwanamke mwenye uzoefu wa umaskini, Tandale, Dar es salaam).

ii. “Sikuweza kuendelea na masomo kwa sababu hapakuwepo mtu wa kunisiaidia; baba yangu alifariki wakati ningali mdogo sana”

(Mzee anayeishi katika mazingira ya umaskini katika maeneo ya Tegeta, Dar es salaam)

iii. “Ni kweli kwamba wazazi wetu walikuwa na maarifa na ujuzi. Walikuwa wanaweza kutengeneza zana mbalimbali kutokana na udongo wa chuma lakini ujuzi na maarifa hayo yamepotea kwa sababu ya kutokuwepo elimu ya kuyaboresha na hivyo kurithishwa kutoka kizazi hadi kizazi”.

(Mzee anayeishi katika umaskini katika wilaya ya Ludewa).

iv. “Ingawa wazazi wangu walikuwa wanamiliki mifugo mingi hawakutaka kunipeleka shule; badala yake walinitaka nikachunge mifugo. Hii ilinifanya nisiende shule kabisa”.

(Mzee anayeishi katika uzoefu wa umaskini, Njombe).

02. Afya Mbovu



Maana: Kipimo hiki kinahusu afya dhaifu ya mwili au akili inayosababisha matatizo ya kiafya.

Maelezo ya kipimo

Afya ni mojawapo kati ya vipimo vinavyochukua eneo kubwa katika umaskini. Watu wanaoishi katika umaskini mara nyingi hukabiliana na mazingira magumu sana ambayo si tu kwamba yanaathiri hali zao lakini pia huingiliana na masuala mengi yanayowahusu. Kwa mfano, afya mbovu hupunguza uwezo wa uzalishaji na kudumaza uwezo wa kutumia maarifa; magonjwa ya kila mara hupunguza kipato cha familia na kusababisha udhaifu katika utendaji wa mwili na pengine kusababisha vifo. Afya mbovu mionganoni mwa watu wanaoishi katika umaskini inaweza kusababisha madhara mengi kama vile, kushindwa kupata huduma za kiafya kwa sababu ya ubovu wa miundo mbinu ya barabara, upungufu wa madawa katika vituo vya afya, kushindwa kugharamia matibabu, kukosa dawa husika, chakula kisicho na lishe (kukosa lishe stahiki), kufanya kazi ngumu na hatarishi, mazingira duni ya kuishi, ajali, kuzeeka mionganoni mwa mengine. Kuzeeka kunahusiana sana na kozorota kwa afya. Wazee wanaoishi katika umaskini afya zao hutegemewa kuwa mbaya zaidi kuliko wanaoishi katika mazingira ya aina nyingine. Vipengele vyote hivi huwafanya watu wanaoishi katika umaskini kuwa maskini zaidi.

i. “Katika uhalisia, huduma za afya ziko mbali sana kutoka katika makazi yetu. Kijijini kwetu ni hali ya kawaida kuwaona wanawake wajawazito wakipoteza watoto wakati wa kujifungua, hawana usafiri wa kwenda hospitali kwa ajili ya kujifungua salama”.

(Mtu mzima mwenye uzoefu wa umaskini, Kata ya Keikei, Kondoa, Dodoma).

ii. “Zamani kulikuwa na tabia nzuri na nidhamu katika ulaji wa vyakula. Aina ya vyakula ambavyo vilikuwa haviliwi na wanawake na aina zingine za vyakula vilikuwa haviliwi na wanaume. Pia wanawake walikuwa wanatumia vikapu vya asili kubebea mboga za majani kutoka mashambani kwao. Lakini siku hizi haya hayafanyiki. Mboga za majani zinabebwa katika mifuko na vyombo ambavyo hata havifahamiki. Tabia za ulaji zimebadilika; ndiyo maana tunapata magonjwa ya mara kwa mara”.

(Mzee mwenye uzoefu wa umasikini wilaya ya Ludewa, mkoani Njombe).

iii. ”Unapozeeka unaanza kupata madhara mbali mbali kama vile kutokuona vizuri, maumivu ya mwili na kukosa nguvu ya kufanya kazi za uzalishaji. Unakuwa tegemezi.

(Mzee mwenye uzoefu wa umaskini, wilaya ya Ludewa).


iv. “Hapa katika kata yetu, unapougu na kwenda katika kituo cha afya, tabibu anakuandikia dawa. Unapokwenda kuchukua dawa unaambiwa dawa zimekwisha. Katika famasia za binafsi dawa ni ghali sana, bei yake hatuiwezi”

(Mzee mwenye uzoefu wa umaskini katika kata ya Luvuyo wilayani Ludewa).

v. “Jirani yangu mwanamke aliugua sana na akaamua asiende hospitali kwa sababu hakuwa na fedha ya kugharamia matibabu. Jirani yake mmoja msamaria mwema alijitolea kuzunguka kila nyumba kumchangia fedha ili waweze kumpeleka hospitali kwa ajili ya matibabu. Fedha kiasi ilipatikana na akapelekwa hospitali ambako alipata matibabu na kupona. Lakini miezi kadhaa baadaye aliugua tena na kufariki”

(Mwanamke mwenye uzoefu wa umaskini, Tandale, Dar es salaam).

03. Umaskini wa Kipato



Maana: Kipimo hiki maana yake ni kuwa na kipato kidogo kiasi cha kushindwa kugharamia mahitaji ya msingi na majukumu ya kijamii. Kuwa na kipato huleta amani na utulivu katika familia na kufurahia mazingira mazuri ya maisha

Maelezo ya kipimo

Bila pesa ya kutosha ni rahisi kuingia katika madeni kwa lengo la kufanikisha upatikanaji wa mahitaji ya msingi na hivyo kuingia katka lindi la kuwategemea wengine na matokeo yake ni kujihatarisha kunyonywa na kuwa katika hali mbaya kiuchumi. Wakati mwingine kipato cha watu wazima huwa kidogo sana kiasi kwamba watoto wao hulazimika kufanya kazi ili waweze kusaidia familia. Kazi hizi zinaweza kuwaweka watoto katika mazingira hatarishi na katika hatari ya kudhalilishwa.

- i.** “Niliacha shule nilipokuwa darasa la nne kwa sababu wazazi wangu hawakuweza kuninilipia ada ya shule na mahitaji mengine”.

(Mtu mzima mwenye uzoefu wa maisha ya umaskini, Kipawa, Dar es salaam).

- ii.** “Nakumbuka namna umaskini ulivyoleta mateso katika familia yangu kiasi kwamba mume wangu akalazimika kwenda Msumbiji kutafuta kazi, nchi ambayo alikuwa hajawahi kufika, kutafuta kazi ambayo hakuwa na uhakika wa kuipata. Aliishia kupata mateso zaidi akifanya kazi hatarishi kuweza kujikimu ili aweze kuishi, hatimaye alirejea nyumbani mikono mitupu”.

(Mwanamke mwenye uzoefu wa umaskini,Tandale).

- iii.** “Wazazi wangu walipoachana niliishi maisha magumu sana hivyo ikanilazimu niache shule na kufanya kazi katika machimbo kama mvunja mawe nikitumia baruti. Siku moja baruti ililipuka na kuharibu nyumba iliyokuwa jirani. Nililazimika kuuza kiwanja changu kwa bei ya chini ili niweze kuikarabati. Leo hii nimebaki maskini na kazi hii ninayoifanya wala haiwezi hata kunitimizia mahitaji yangu ya siku. Nimebaki maskini kabisa”.

(Mtu mzima mwenye uzoefu wa umaskini, Boko, Dar es salaam).

iv. “Tunafanya kazi kuliko uwezo wetu na tunalipwa kidogo kuliko ugumu wa kazi tunayoifanya. Wanawake wengi wanaofanya kazi katika machimbo huamka saa kumi na moja alfajiri, hufanya kazi kuanzia saa kumi na mbili hadi saa kumi jioni. Mwisho wa siku wanapata kiasi cha shilingi elfu mbili hadi shilingi elfu tano tu”.

(Mwanamke mwenye uzoefu wa umasikini anayefanya kazi ya kuvunja mawe katikamachimbo ya Boko).

v. “Tunapovunja mawe, mengine ni mazito sana kuyanyanya juu ya vichwa vyetu hali amabayo wakati mwengine hutusababishia majeraha katika miili yetu. Nilipoanza kufanya kazi hii nilikuwa na mume wangu lakini baada ya miaka miwili alipata kifua kikuu. Sasa hawezi tena kufanya aina hii ya kazi. Ni mimi ninayelazimika kutafuta riziki kwa ajili ya familia na kumhudumia”.

(Mwanamke mwenye uzoefu wa umaskini kutoka Kunduchi, Dar es salaam).

vi. “Mwanzoni tulifikiria kwamba wanaumwa lakini baadaye tuligundua kwamba ilikuwa ni kwa sababu ya njaa. Pia tuligundua kwamba wengi kati ya hawa watoto wanatoka katika familia zinazokabiliana na umaskini wa kipato na kwamba wanakuwa dhaifu kwa sababu wanalala na njaa. Hawapati kifungua kinywa hivyo wanakuwa dhaifu”.

(Mwalimu kutoka shule ya msingi Tegeta, Dar es salaam)

vii. ”Baadhi ya wanafunzi wanakuja shulenii na kaptura zilizochanika kwa hiyo hawawezi kuchomekea mashati yao. Mwalimu anakuja na kuwaadhibu bila kujua kwamba wanafanya hivyo kuepuka aibu (kuficha kaptura zao zilizochanika nyuma) kwamba wanafanya hivyo kwa sababu hawana nguo za ndani. Vivyo hivyo wanaotoka katika familia maskini wanaletwa hospitali wakionekana kuwa wagonjwa sana lakini kumbe ni kwa ajili ya njaa, Wanapoandikiwa dawa hawamezi mbele ya daktari kwa sababu tu kwamba matumbo yao yanakuwa hayana cho chote.

(Mwalimu kutoka Tegeta shule ya msingi, Dar es salaam).

Vipimo Vya Umaskini Vilivyofichika Kutoka Katika Mikoa Mitano ya Tanzania Bara

Vipimo hivi vimetajwa na watu wanaoishi katika umaskini kwamba ni muhimu kutokana na uzoefu wao wa maisha, lakini kwa kiasi kikubwa vimekuwa vinapuuzwa. Wanasaikolojia, waethonolojia na hata wachumi wanavifahamu sana lakini vinachukuliwa kwamba vimefichika kwa sababu vimekuwa havitambuliwi kwa maana kwamba havijapewa uzito katika idadi ya viashiria vya maendeleo kama vile dola 1.9 kwa siku au (HPI au MPI). Kwa sababu hiyo havijatambuliwa katika mijadala ya kisiasa. Kwa hiyo namna vipimo hivi vinaavyoingiliana kutengeneza uzoefu wa umaskini bado haijaeleweka vizuri

01. Mazingira na Makazi Duni



Maana: Kipimo hiki kinahusu mahali watu maskini wanapoishi pamoja na aina ya makazi wanayomiliki. Baadhi ya maeneo haya yanahuisha makazi dhaifu na yaliyosongamana, yakiwa hayana huduma za afya; aina za nyumba (aina ya paa na vifaa vilivyotumika kujengea paa na kuta, zana hafifu bila ubora); mazingira yanayozungukia makazi hayo (mara nyingi yakiwa machafu, mifereji ya maji machafu yaliyotuama).

Maelezo ya kipimo

Watu wanaoishi katika uzoefu wa umaskini hulazimika kuishi katika mazingira mabaya. Kwa watu wengi makazi wanayoishi huwakilisha asili ya maisha yao. Lakini hali halisia ni kwamba mahali wanapoishi watu maskini hukabiliana na aina kadhaa za kutengwa; kukosa miundo mbinu; huduma kama maji safi ya kunywa, huduma za usafi na afya, shule kwa ajili ya watoto wao; uchafuzi na uharibifu wa mazingira; kukabiliana na majanga kama mafuriko na mmonyonyoko wa ardhi. Majanga ya kimazingira huwafanya wasiwe na utulivu kwa ajili ya usalama wao.

Familia nyingi za kipato cha chini zinaishi katika nyumba zilizo katika hali mbaya (dhaifu, zimechoka) katika mazingira yasiyofaa bila huduma za msingi. Tatizo ya mahali pa kuishi limekuwa ndilo tatizo kubwa linaloleta msongo katika maisha ya familia zinazokabiliana na mazingira magumu hususani watoto. Kutokuwa kwao na uwezo wa kifedha kunawafanya wasiweze kuboresha makazi yao au hata kuhamia maeneo bora na salama.

Shuhuda kutoka vikundi rika vya watoto zilionesha gharama kubwa za mazingira duni na makazi yasiyofaa kwa hali zao, afya zao na pia kwa afya zao na mahusiano yao kijamii. Kwa watoto, nyumbani ni chanzo cha msingi kwa utulivu wa mwili na akili, usalama wao na wa vitu vyao, mahali pa mahusiano imara ya kijamii. Makazi yao ya muda husababisha ugumu katika mazingira yao ya kupata chakula, kulala, kupata faragha na maeneo ya kucheza. Mara nyingi makazi yao ni duni na finyu, wakiyatumi kwa huduma kama vile kunawa, kula, kuoga, matumizi ya maliwato na kulala pamoja watu wengi bila faragha yo yote. Kutokana na utafiti tunajua kwamba watu wanaoishi katika umaskini wanapambana kuwalinda na kuwasaidia watoto wao, wakikabiliana na madhila yote haya. Baadhi ya nukuu zifuatazo kutoka kwa watu wanaoishi katika uzoefu wa maisha ya umaskini zinaonesha namna maisha yanavyokuwa magumu zaidi pale yanapouunganishwa na hali ya kuishi katika mazingira duni na katika nyumba zilizo dhaifu na duni.

i.

“Tunaishi katika nyumba zinazokaribia kuanguka, zikiwa zimejengwa kwa miti bila matofari, ambazo kuta zake zimeinamia upande mmoja. Kuta zinauliza;’Tukuue leo au kesho?’ Nasi tunajibu; ‘Tafadhali subirini kidogo, bado tunatafuta msaada””.

(Mtoto anayeishi katika uzoefu wa umaskini kutoka Rubuga, Kigoma).

ii.

“Nyumba pekee isiyoweza kufikiwa iko katika takataka, hakuna usalama na imejengwa katika eneo ambalo hupata mafuriko”.

(Mtu mzima kutoka kipawa Dar es salaam).

iii.

“Tunaishi katika chumba kidogo kisicho na nafasi, hakina faragha wala hupati muda wa faragha”

(Mwanamke kutoka Tandale, Dar es salaam).

02. Ushirikiano wa Watu Wanaoishi katika Umaskini



*Maana: Kipimo hiki kinahusu mikakati ya kukabiliana
iliyotumiwa na watu wanaoishi katika umasikini katika
kusaidiana kwa vitu au kimawazo na katika shida kwa kupeana
moyo wakati wa uhitaji.*

Maelezo ya kipimo

Watu wanaoishi katika umaskini hupenda kusaidiana wao kwa wao kidogo walichonacho, wakijipunguzia hicho kidogo walichonacho hali ambayo inaendelea kuwazamisha katika lindi la umaskini. Hata hivyo tabia hii huwapa ujasiri na matumaini ya kuendelea kuishi na hisia za kushirikishana mapambano na mshikamano, hali ambayo huwasaidia kuepukana na kukata tamaa na mawazo ya kujitoa uhai. Mifano ni kama vile kupeana chakula, kuazimana nguo na vyombo vya nyumbani, kupanga mikusanyiko ya kijamii pamoja na kushirikiana katika kazi za pamoja kama vile vikundi vya kusaidiana kulima au katika msuala kama vile ya harusi.

i.

“Wakati fulani hatukuwa na chakula nyumbani na tulikuwa tumelala njaa kwa muda wa siku mbili. Mama yetu aliamua kwenda kuomba chakula kwa jirani ambaye naye aliamua kugawana nasi kidogo alichokuwa nacho bila kujali kitakachotokea siku itakayofuatia”.

(Mwanaume mmoja kutoka Boko Tegeta)

ii.

“Binti yangu alikuwa anamaliza darasa la saba. Nilikaribishwa kuhudhuria mahafali yake. Nilikuwa nimeamua kutokwenda kwa sababu sikuwa na vazi la kufaa kwa ajili ya shughuri kama hiyo. Jirani yangu aliniuliza kwa nini nilikuwa siendi kwenye mahafali, nilimwambia kwamba sikuwa na vazi la kufaa. Aliamua kuniazima vazi lake nikaweza kuhudhuria katika mahafali ya binti yangu.

(Mwanamke katika uzoefu wa umaskini wilaya ya Kondoaa)

03.

Ukatili, Unyanyasaji na Ukandamizaji dhidi ya Wanawake na Watoto



Maana: Kipimo hiki kinafafanua namna wanawake na watoto wanavyofanyiwa katika jamii, hususani katika mazingira yanayohusiana na umaskini.

Maelezo ya kipimo

Katika mazingira ya umaskini, wanawake na watoto ndiyo makundi yasiyo salama zaidi. Wanapata shida kutokana na jinsi wanavyotendewa vibaya na jamii hali ambayo inatokana na ukiukwaji wa haki za binadamu. Kwa mfano dhuluma kwa wajane, kutowaruhusu wanawake kufanya maamuzi, kuwalazimisha watoto kufanya kazi, kulazimisha wasichana kuolewa katika umri mdogo na kutoa adhabu zinazoumiza kama vile viboko, kote nyumbani na shulen. Watoto wanatumika nyumbani kama nguvu kazi na wanapokwenda shulen wakiwa wamechelewa au/na wakiwa wamechafuka huadhibiwa. Hizi zote ni shida na mateso katika maisha ya watoto na wanawake. Hali hii inaweza kuchagizwa na mila na desturi potofu katika jamii; imani potofu; utekelezaji dhaifu wa sheria zinazolinda watoto na wanawake katika ngazi za serikali za mitaa.

Wanawake wanaponyang'anywa haki zao wakati wa mchakato wa talaka (mali zilizopatikana wanandoa walipokuwa wakiishi pamoja), wanakuwa hawana uhuru wa kuchagua wala kuchangia mawazo yao. Wanapewa uwezo mdogo sana wa maamuzi. Wanalazimishwa kuingia katika umaskini hali ambayo imekuwa chanzo kikubwa cha umaskini kwa wanawake wengi. Pia wanateseka kwa kukosa usawa katika mgawanyo wa mali na usawa kati yao na wanaume katika jamii. Kwa mfano, katika mila nyingi umiliki wa ardhi, mirathi na fursa za elimu kwao ni kikwazo. Wanawake wanazuiwa na waume zao kufanya kazi za kuajiriwa na pia wanabanwa na mfumo dume. Hii inawahusu wanawake wote masikini na wanaotoka katika jamii tajiri. Lakini wanawake wanoishi katika umaskini wanaathirika zaidi kwa sababu hali hii inaondoa kabisa juhudu zao za kujiondoa katika umaskini na hivyo kuwafanya watumbukie katika umaskini uliokithiri.

i.

“Wapo wanawake wengi ambao wanazuiwa na waume wao fursa na uhuru wa kuajiriwa. Wengine wanazuiwa hata kijiungu na vikundi vyatia kiuchumi vyatia kina mama kupata fedha ambayo ingweza kusaidia katika familia zao.Hii ni kutokana na mila na tamaduni”

(Mwanamke anayeishi katika uzoefu wa umaskini, soko la samaki Ferry, Dar es salaam).

ii.

“Binti zangu walizuiwa na baba yao kuhudhuria shule kwa sababu alifikiria kwamba ni kupoteza rasilimali na alikuwa na hisia kwamba siku moja wataolewa katika familia zingine ambazo ndizo zitakazofaidika na siyo baba ambaye alikataa kuwasomesha”.

(Mwanamke mwenye uzoefu wa umaskini katika wilaya ya Bahi, Dodoma).

iii.

“Sisi wanawake tunafanya kazi mashambani kuzalisha na kuleta pato na pia tunazaa watoto. Wanaume wanakaa tu na kunywa kahawa na kuongea. Wakati wa mavuno baada ya wanawake kuuza mazao yote, wanaume huchukua pesa yote na kuitumia na kuoa mwanamke mwingine....Ni jamii ambayo mwanamke hana maamuzi”.

(Mwanamke mtaalamu, Kondoa, Dodoma).

iv.

“Wasichana wananyimwa haki yao ya kupata elimu. Wakati watoto wa kiume wanapelekwa shule, mabinti wanaozeshwa. Hata wanapoozeshwa hupewa maelekezo kuwatii na kuwaheshimu waume zao, nao inawapasa kufuata maelekezo hayo. Katika hali hiyo mwanamke anakuwa mfungwa wa mila na desturi mbovu”.

(Mwanamke mzee mwenye uzoefu wa umaskini, Boko, Dar es salaam).

v.

“Mwanamke anakuwa tegemezi kwa mume wake, na endapo mwanaume hawezikupata pesa mwanamke anabaki na njaa. Ni vema mwanamke apate elimu kwa kuwa naye atakuwa na uwezo wa kusaidia familia....” Anaangua kilio na anashindwa kuendelea...

(Mwanamke mtu mzima anayeishi katika uzoefu wa umaskini, soko la samaki, Dar es salaam).

04.

Mmomonyoko wa Maadili



Maana: Kipimo hiki kinafafanua namna watu wanaoishi katika umasikini wanavyoweza kuathiriwa na kupata shida katika ngazi ya mtu binafsi, ngazi ya familia au katika ngazi ya jamii.

Maelezo ya kipimo

Watu wanaoishi katika umasikini huzama zaidi katika lindi la umaskini kwa sababu ya kushindwa kutambua namna ya kwenda sambamba au kukubali kuyaishi maadili katika jamii kama inavyojitokeza katika hali zao za mmomonyoko wa maadili. Hizi zinaweza kuwa kichocheo au matokeo hasi ya umasikini kwa watu wanaoishi katika uzoefu wa umasikini.

Watu wanaoishi katika umaskini wanapokuwa waraibu wa pombe, dawa za kulevyta, Kamari na sherehe zisizo na umuhimu wanajihatarisha kuzama zaidi katika umaskini uliokithiri kwa sababu hutumia vibaya rasilimali kidogo walizonazo ambazo zinaweza kuwaondoa katika umaskini. Watu wanaoishi katika umaskini wako katika hatari pia ya kuangukia katika maadili mabaya kama vile uvunjaji wa sheria, uvivu na kukimbia familia. Pia wanaweza kukosa uaminifu, uwazi na uwajibikaji hususani wale wanaopewa majukumu na serikali ili wafanye kazi pamoja na watu wanaoishi katika umaskini hasa katika programu za maendeleo.

i

“Nilipokuwa kijana nilipata pesa nyingi rafiki yangu mmoja alinishawishi kucheza Kamari matokeo yake nilipoteza pesa yangu yote. Baada ya hapo nilianza kusababisha matatizo nyumbani na kumpiga mke wangu kwa sababu nilikuwa namkasirikia kila mtu, hatimaye nikaishia kuwa mraibu wa pombe”

(Mtu mzima mwenye uzoefu wa umaskini uliokithiri, soko la samaki, Dar es salaam).

ii.

“Kwetu, tunayo desturi ya kumweka binti ndani anapofikia umri wa kuvunja ungo. Anafichwa ndani, hupewa chakula na maelekezo namna ya kuhudumia familia hususani mumewe pale atakapoolerwa. Nawafahamu watu waliouza viwanja vyao kwa ajili kutekeleza shughuri ya namna hii. Shughuri hizi ni nyingi na watu hutumia pesa nyingi sana”.

(Mwanamke mwenye uzoefu wa umaskini kutoka Feri)

iii.

“Siku moja nilipata kazi ya kibarua shambani kwa jirani yangu. Nilipokuwa naendelea kufanya kazi shambani, aliniletea chakula bila kuniambia kwamba atanikata katika malipo yangu. Baada ya kula chakula ndipo aliponiambia kwamba atanikata kutoka katika mshahara wangu bila kuniambia atanikata kiasi gani”.

(Mjane mwenye uzoefu wa umaskini, Bahi, Dodoma).

iv.

“Mimi pamoja na mwenzangu tulikwenda kuomba kazi. Mwenye shamba akatuambia atatulipa shilingi elfu ishirini kwa kulima ekari moja. Alituambia kwamba ni ekari moja tu, lakini alikuwa ametudanganya kwa sababu lilikuwa zaidi ya ekari moja na ingetuchukua zaidi ya siku tano kumaliza kazi yote. Tulijaribu kufanya kazi siku ya kwanza. Siku ya pili tuliachia kila kitu bila kumwambia mwenye shamba kwa sababu tulitambua kwamba hatutapata haki yetu”.

(Mwanamke mwenye uzoefu wa umaskini, Bahi, Dodoma).

05. Mila na Desturi Potofu.



Maana: Mila na desturi zinaakisi thamani ya tamaduni na imani ambayo imekuwa inafuatwa na jamii miaka kwa miaka, vizazi kwa vizazi. Lakini ndani ya mila hizi zipo zile zinazoleta matokeo hasi kwa mtu binafsi na katika jamii.

Maelezo ya kipimo

Jamii tofauti hapa Tanzania zina tamaduni, mila, desturi na imani tofauti, baadhi yake zikiwa na manufaa kwa wanajamii husika na baadhi siyo nzuri kwa makundi fulani katika jamii kama vile wanawake, walemovu na wasichana. Mila hizi potofu zina athari ambazo huchangia katika kuleta umaskini, nazo ni kama vile ndoa za utotonii, imani za kichawi, mahari na upendeleo kwa watoto wa kiume dhidi ya watoto wa kike. Katika kipimo hiki washiriki walijihuisha zaidi na imani za kichawi. Imani za kichawi zimeenea sana na zinatumika kuleta bahati mbaya au njema

(Is Witchcraft New Enemy to Our Country? – Tanzania Daily News, 23 February 2019).

Katika maeneo mengi nchini Tanzania, Imani Potofu inamaanisha matumizi ya uchawi, ambapo baadhi ya watu katika jamii wanaamini kwamba wanaweza kufanikiwa na kupata mali nyingi kwa gharama ya watu wengine. Kiasi kikubwa cha fedha zinazotumika katika masuala ya imani za kishirikiana kinaleta athari kubwa katika bajeti za familia. Imani hizi zinaleta matokeo hasi kwa baadhi ya makundi katika jamii. Makundi haya ni kama vile walemovu wa ngozi, akina mama wazee walio na macho mekundu, walemovu na vijana ambao wamehusishwa katika mauaji yanayohusiana na imani hizi za kishirikina katika maeneo mengi nchini Tanzania. Matukio ya watoto kutekwa na kupotea yamekuwa yanaongezeka kwa kasi nchini na yote yanahuishwa na Imani potofu. Mifano mingine ni pamoja na mauaji ya walemovu wa viungo: mauaji ya vijana wadogo katika maeneo ya Njombe na Simiyu ambayo yanatokana na imani kwamba kwa kutumia viungo vya siri vya watu katika masuala ya ushirikina hii inaweza kuleta bahati au mafanikio katika shughuli za mtu au katikabiashara.

(Tanzania Daily News 23 February, 2019).


i. “Tabia ya kujishirikisha katika Imani za kishirikina huzifanya familia nyingi kurudi nyuma katika masuala ya maendeleo. Kwa sasa jamii inakabiliana na changamoto ya mauaji ya makundi yaliyo katika hatari hususani watu wenyewe ulemavu wa ngozi kwa sababu wengi wanaamini kwamba kwa kutumia viungo vyao wanaweza kupata utajiri. Suala la mauaji ya namna hiyo limesababisha matatizo mengi na taabu kwa wanajamii kiasi kwamba serikali imechukua hatua kali kuwalinda watoto walio na ulemavu wa ngozi na kuwaweka katika kambi na vituo maalumu. Hata hivyo licha ya hatua zote hizi bado watu wenyewe ulemavu wa ngozi wanawindwa usiku na kuuawa nyumbani kwao”.

*(Mwanamke mwenye uzoefu wa umaskini, soko la samaki,
Dar es salaam)*

ii. “Katika mazingira yetu imani za kishirikina zimeenea sana hivi kwamba watu hutegemea kwenda kupiga ramli kutafuta nani anayemfanyia vibaya. Waganga wengi wamekuwa wachonganishi katika jamii na hivyo kusababisha magomvi na kutokuelewana ndugu kwa ndugu, jirani kwa jirani na hivyo kusababisha magomvi katika jamii kila siku”

(Mtu mzima mwenye uzoefu wa umaskini, Kipawa).

06. Mapungufu katika Utekelezaji wa Sera za Taasisi.



Maana: Mapungufu katika utekelezaji wa sera za kitaasisi ni kushindwa kwa vyama vya kijamii na taasisi za kitaifa kupitia katika utekelezaji wake au kushindwa katika utekelezaji wake, kuitikia kwa ukamilifu na kwa hali stahiliki kwa mahitaji na hali za watu wanaoishi katika umaskini kwa kutowajali na kuwafedhehesha na pengine hata kuwadhuru.

Maelezo ya kipimo



Taasisi rasmi za umma na za binafsi, hutengeneza mitazamo hasi kuhusu uzoefu wa umaskini kupitia katika maelezo yake kwa umma na katika utayarishaji na utekelezaji wa sera na huduma na pia kupitia katika kutowajali kwao, na kushindwa kuwasikiliza watu hawa wanaoishi katika umaskini. Wakati baadhi ya taasisi zimechukua dhamana ya kuutokomeza na kuboresha maisha ya watu lakini mara nyingi zinashindwa kufanya hivyo. Wakati mwingine hii maana yake ni kuishi na matokeo hayo ya serikali kushindwa katika utekelezaji wa sera na sheria zilizopo, kutokuwa na usawa katika utoaji wa rasilimali na huduma, na udhalimu usiokoma, ukandamizaji na kunyamazishwa watu wanaoishi katika umaskini. Maana yake pia ni kutokuwa na haki wala sauti katika maamuzi yanayofanywa na taasisi au katika vyama vyaa kijamii.

Katika utengenezaji wa sera, taasisi hupendelea kukuza na kutengeneza mitazamo ya kibaguzi badala ya kukabiliana nayo. Vivyo hivyo, ubunifu na utekelezaji wa sera unaweza kusababisha matokeo ya watu wanaoishi katika umaskini kutengwa na kushindwa kufikia matakwa yao ya msingi. Kwa kuwanyanyapaa, mara nyingi watu wanaoishi katika umaskini huona kwamba kushirikiana kwao na taasisi kunakuwa na mazingira ya kuhukumiwa, kuamuriwa, kushurutishwa, na udhibiti unaokomesha sauti zao na matokeo yake ni kunyimwa haki zao.

i.

“Viongozi kijijini kwetu wameweka kodi nyingi zinazotuathiri. Chochote unachochukua kwenda kuuza sokoni kinalipiwa kodi hata kama hakijauzwa. Kwa mfano, siku ya mnada, unapomchukua mbuzi kwenda kumuuzza kwa ajili ya kupata pesa ya kusaidia familia, unapoingia mnadani unapaswa kulipa kodi. Usipomuuza, unapotoka nje ya eneo la mnada unapaswa kulipa kodi tena. Hii inatuathiri sana.


(Mtu mzima katika uzoefu wa umaskini, Dodoma).

ii.

“Katika maeneo yetu tuna changamoto kubwa sana; kuna ugomvi mkubwa sana kati ya wakulima na wafugaji. Wafugaji wanaamini kwamba ng’ombe wao ni muhimu kuliko mazao yetu. Wachungaji huwaswaga ng’ombe wao kuingia katika mashamba yetu na kula mazao yetu. Hili ni tatizo kubwa sana na ndiyo mgongano wetu mkubwa”.

(Mtu mzima katika umaskini, Kondoa, Dodoma).

07. Kilimo kisichokuwa na Tija



Maana: Kipimo hiki kinahusu vikwazo wanavyokabiliana navyo wakulima wadogo wadogo katika maeneo ya vijiji ambavyo huwazuia kufaidika kutokana na kilimo.

Maelezo ya kipimo

Kiasi cha asilimia 88 ya watu maskini nchini Tanzania wanaishi vijiji. Theluthi mbili ya nguvu kazi nchini Tanzania kwa sasa inajihuisha na kilimo (Mamlaka ya Takwimu, 2015; Osario et al, 2014), lakini hawana mazingira yanayofaa kuwafanya waongeze uzalishaji unaoweza kukifanya kilimo kuwa na tija kwao. Watu wengi wanaoishi katika umaskini wanajihuisha na kilimo cha kujikimu ambacho huwapatia tu chakula na hakiwasaidii chochote zaidi. Aina hii ya ukulima imewafanya wanabaki katika lindi la ufukara.

Utafiti huu umeonesha kwamba wakulima wadogo wadogo wana uhitaji mkubwa sana wa huduma za ughani na mafunzo ili kuweza kuboresha kilimo chao, lakini maafisa ughani ni adimu katika maeneo mengi ya vijiji. Changamoto nyingine kubwa ni ughali wa pembejeo na ukosefu wa masoko ya kuaminika na ukosefu wa taarifa za bei, utegemezi wa mvua wakati majira ya mvua hayatabiriki, athari hasi za mabadiliko ya mazingira na mazingira yao wakulima wadogo wadogo. Pia lipo tatizo la ukosefu wa maji ya kumwagilia, ukosefu wa ardhi na utegemezi wao kwa madalali wa mazao. Mara nyingi huwapunja kwa kuwapatia bei ndogo na kutumia mizani isiyo sahihi. Kwa kuwa wakulima wengi hawana ujuzi wa kujadiliana bei za mazao, kuongezea na mbinu dhaifu wanazotumia katika kilimo, hatimaye huishia kuwa tegemezi zadi kwa madalali wakati wa kuuza mazao hivyo huishia kupata hasara. Vikwazo vyote hivi hufanya kilimo chao kisiwe cha tija kutokana na uzalishaji mdogo wa mazao yasiyo na ubora. Chochote kidogo wanachozalisha, hukabiliana na changamoto lukuki kama vile; kukosa masoko, bei ndogo, miundombinu dhaifu ya barabara kusafirishia mazao yao ili kuweza kufikia masoko sahihi. Kwa hiyo, watu wanaoishi katika uzoefu wa umaskini, wanaona kwamba kilimo siyo njia sahihi ya kuwanasua katika umaskini uliokithiri. Bado wanateseka kutokana na umaskini wa kipato. Asilimia 40 ya wakulima bado wanaishi chini ya mstari wa umaskini wa mahitaji ya msingi (Osario et al, 2014), wakikabiliana na upungufu wa mara kwa mara wa chakula.

Licha ya matatizo yote haya, sekta ya kilimo nchini Tanzania inaendelea kuchangia kiasi kikubwa katika mapato ya nchi ikichangia asilimia 29 kwa GDP mwaka 2015 (NBS, 2016) na kuajiri asilimia 66 ya Watanzania (Mamlaka ya Takwimu). Kwa kuwa sekta hii ndiyo inayoajiri Watanzania wengi zaidi, juhudhi kubwa za kundoa umaskini zinapaswa zielekezwe katika sekta hii.

i. “Kijijini kwetu hatuna maafisa ughani. Afisa ughani wa kata anakaa makao makuu ya wilaya ambapo ni kilometra 150 kutoka hapa. Anakuja mara moja moja kijijini. Anapokuja halali hapa bali anakuja na kurudi. Pembejeo za kilimo pia hupatikana kwa shida. Tukipata mafunzo ya kilimo na pembejeo, kilimo chetu kitakuwa bora na tutaweza kuondokana na umaskini”

(Mtu mzima katika uzoefu wa umaskini, Keikei, Kondoa).

ii. “Tatizo ni kwamba maafisa ughani hawatoshi. Angalia kwa mfano, mimi ni afisa ughani ninayewajibika kwa kata nzima ambapo natakiwa niwasaidie wakulima katika kata nzima. Inakuwa vigumu kuwafikia wote kwa sababu hatuna usafiri”.

(Afisa ughani kutoka Ludewa, Njombe).

iii. “Wenye fedha huwatumia maskini kwa manufaa yao. Upo unyonyaji wa kiuchumi. Wakulima wadogo wanalazimika kuuza mazao yao kwa bei inayopangwa na wenye fedha wanaotoka mijini. Mara nyingi pia wanachezea mizani ili waweze kunufaika kutoka kwa watu wanaoishi katika umaskini”

(Mwanamke mwenye uzoefu wa umaskini, Bahi, Dodoma)

08.

Unyanyasaji na

Kutengwa

na Jamii



Maana: Kipimo kinaonesha namna watu wanaoishi katika umaskini uliokithiri wanavyonyimwa fursa za kushiriki katika shughuli mbalimbali za kiuchumi, kijamii, kisiasa, kitamaduni katika jumuiya na jamii zao.

Maelezo ya kipimo

Umaskini ni unyanyapaa mkubwa katika nafasi za kijamii, na maisha ya umaskini katika jamii iliyo na ukwasi yanaweza kuwa ya kutengwa hasa na kusababisha madhara katika kijamii.

Tofauti katika jamii ambazo husababisha kundi moja kutambulishwa kama “wale” likichukuliwa kuwa tofauti na wengine katika jamii kwamba matokeo yao kuwa maskini ni athari mbaya sana katika maisha ya watu. Lister (2004:103) anahoji kwamba, “kuwapa majina au kuwatambulisha watu wanaoishi katika umaskini kama “hao”, “wale” au “wengine” huleta madhara ya kiishara, katika mila na desturi, kisaikolojia na kiumiliki wa vitu”. Masuala haya yanaibuka katika jamii tofauti ambapo watu wanaoishi katika umaskini hukabiliana na ubaguzi na kutengwa katika jamii.

Watu wanaoishi katika umaskini wanayo mahitaji yao ya msingi ambayo ni kawaida kwamba hayazungumzwi katika mipango rasmi ya maendeleo wala hayapewi kipaumbele katika sera za kitaifa kwa sababu maskini wenyewe hawapewi fursa za kushiriki katika mipango ya maendeleo. Ushiriki wao dhaifu, kutokuwa na sauti, ukosefu wa fedha mionganoni mwao na mwelekeo wa ubinafsi katika jamii, huwazuia watu wanaoishi katika umaskini kushiriki kwa ukamilifu katika maendeleo ya uchumi.

Bila ushiriki wao hai hakuna maendeleo shirikishi yanayoweza kufikiwa na matokeo yake ni kwamba umaskini utaendelea kuwepo. Kushuka kwa mshikamano katika jamii na kuperomoka kwa mfumo wa usalama ni sababu kubwa ambazo zimesababisha ongezeko la ubaguzi na kutengwa katika jamii kwa watu wanaoishi katika umasikini uliokithiri na hii inasababisha kuongezeka kwa ufukara.

- i.** “Katika kila shughuli za kijamii kama vile harusi, mimi hutengwa. Kwa kuwa jirani zangu wanajua kwamba siwezi kuchangia cho chote, huwa sikaribishwi katika shughuli zao.

(Mama mjane kutoka Tegeta, Dar es salaam).

- ii.** “Upweke ni mbaya sana. Ninapokuwa na shangazi yangu najisikia furaha. Ingawa shangazi yangu naye ni maskini, najisikia vizuri. Upweke ni mgumu, unajisikia vibaya. Inaumiza sana moyo”.

(Mwanamke mlemavu anayekaa Tandale, Dar es salaam).

09. Ulinzi na Malezi Duni ya Wazazi na Jamii



Maana: Kipimo hiki kinahusu watoto kutoka katika familia maskini wasiopata ulinzi, malezi ya wazazi wala jamii kwa ujumla.

Maelezo ya kipimo

Ingawa suala la ulinzi na malezi kwa watoto linahusu pande zote, walio katika uzoefu wa umaskini na wasio, kipimo hiki kimsingi kinalenga kuwaangalia watu wanaoishi katika umaskini. Umasikini uliokithiri husababisha wazazi kukosa utulivu. Wazazi hutumia muda wao mwangi pengine hata siku nzima wakitafuta cho chote cha familia kupeleka kinywani kwa sababu hawana vyanzo rasmi nya mapato. Watoto katika hizi familia huishia mitaani kutafuta chakula na kuomba omba, pengine hujihusisha na ukahaba, madawa ya kulevyta na wizi. Hii inatokana na sababu kwamba mara zote wazazi wao wanakuwa hawapo na huwaacha wakiwa hawana chochote cha kula pia bila ulinzi wa aina yoyote. Inaweza pia kutokea kwa watoto wanaoishi katika vituo nya malezi ya yatima. Vituo hivi vinaweza kushindwa kutoa malezi au matunzo sawa na mtoto anayeolewa katika familia. Watoto hukosa upendo na malezi ya wazazi, hivyo huathirika kisaikolojia na hii huathiri makuzi yao na maisha yao ya utotoni.

Wanajamii hawaoni kwamba kumwangalia mtoto wa jirani ni jukumu la kila mmoja. Hii inatokana na sababu kwamba mfumo wa ulinzi wa jumuiya katika jamii mahalia umeporomoka na pia sheria zinazosimamia ulinzi wa watoto hazisimamiwi inavyopasa katika ngazi za mitaa na jumuiya zake husika. Kwa mfano suala la kutekwa nyara na kupotea watoto ni kwa sababu ya hali hii dhaifu katika uwajibikaji na mifumo ya ulinzi isiyordhisha katika jamii.

i.

Naishi na mama, baba amefariki, nasomeshwa na mama ambaye hufanya kazi ya kugonga mawe. Ndugu wa baba hawamsaidii mama kunilea. Mfano : Inapotokea michango ya shule, inanipasa kugonga mawe ili nipate ada ya matumizi mengine ya shule.

*(Mtoto mwenye uzoefu wa umaskini
- Boko, Dar es salaam).*

ii.

Nafanya kazi zote nyumbani, Naosha vyombo, nasafisha nyumba, nachunga mifugo. Nikisema nimechoka naadhibiwa

*(Mtoto mwenye uzoefu wa umaskini kutoka Kibondo,
- Kigoma).*

10. Athari za Kisaikolojia zinazosababishwa na Umaskini



Maana: Athari za kisaikolojia zinazosababishwa na umaskini ni matokeo ya moja kwa moja ya umaskini uliokithiri yanayotokana na mateso na ugumu wa maisha.

Maelezo ya kipimo

Kuishi katika umaskini uliokithiri kunamaanisha kupata mateso ya kimwili, kiakili pamoja na hisia za kujiona huwezi kufanya lolote kuhusu hali hiyo. Mateso na maisha magumu ni pamoja na fikra hasi ambapo kunakuwa na hisia mbaya zinazoweza kutawala nafsi na matokeo yake yanaweza kumzidia mhusika na kumwondolea amani ya nafsi, kusababisha wasiwasi na uoga usiokwisha kuhusiana na hatima yake; shinikizo na wasiwasi kutokana na kuhangainia yasiyoeleweka, aibu inayohusiana na mazingira na aina ya maisha anayoishi na uhitaji wa kuhitaji msaada, maumivu yasiyovumilika kwa kumpoteza mpendwa na kutengana na watoto; kukata tamaa na kupoteza matumaini wakati inapokuwa hakuna uwezekano wa kuondokana na umaskini. Haya yote yanaweza kusababisha ongezeko la kukata tamaa, hasira, huzuni na kupoteza tumaini matokeo yake yakiwa ni kujikataa au hata kujitoa uhai. Kutafuta nafuu kwa kutumia madawa ya kulevyaa ni nafuu ya muda mfupi katika kujipumzisha na mateso. Watu wanapokabiliana na mateso namna hii kila siku na kunyimwa haki ya utu wao hakika wanakosa heshima wanayostahili.

Wazazi wanateseka, watoto wanateseka, kila mmoja anateseka kwa ajili ya mwenzake.

Mateso namna hii husababisha mengine zaidi kusababisha maisha yasiweze kuvumilika. Ukali wa mateso unasababisha watu kukwepana na kuogopa kuhukumiana ama kuoneana aibu hali ambayo matokeo yake ni kujitenga au kutengwa na jamii na hivyo kusababisha makovu ya kisaikolojia.

i. “Sijui nifanye nini kwa ajili ya wanangu miye. Nina wasiwasi sana kuhusu hatima yao. Ninapowaona wanakuja hapa shimoni kuvunja mawe pamoja nami siku nzima, natafakari juu ya hatima yao. Kusema kweli hili linanipa mawazo kiasi kwamba pengine nakesha usiku kucha bila kulala”

(Mwanamke anayeishi katika uzoefu wa umaskini katika machimbo ya Boko).

ii. “Kukosa ujasiri wa kuanzisha cho chote kipyä ikiwa pamoja na biashara, hofu ya kutengwa inamfanya mtu ajishushe mno, ajidharau na kujiona kwamba hayuko sawa na wengine”.

(Mtu mzima anayeishi katika uzoefu wa umaskini, Kipawa, Dar es salaam).

iii. “Sina hakika kuhusu hatima yangu. Sijui kama kesho nitapata chochote kwa ajili ya mlo.. Sielewi chochote kuhusu itakuwaje kesho. Sina uhakika nitaishije”.

(Mtu mzima anayeishi katika uzoefu wa umaskini kutoka Tandale, Dar es salaam).

HITIMISHO NA MAPENDEKEZO



Kipengele hiki kinawasilisha maamuzi na mapendekezo mbalimbali ya sera ambayo yanaweza kuwa na manufaa kwa watunga sera wa kitaifa na kimataifa. Kama vile ilivyodokezwa awali, mapambano dhidi ya umasikini ndilo lengo la kwanza katika Malengo Endelevu ya Maendeleo kama yalivyokubaliwana Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa mnamo Septemba 2015. Vivyo hivyo mapambano dhidi ya umasikini ni mojawapo ya vipaumbele vya kwanza katika Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano wa Tanzania (FYDPII), 2016/2017-2020/2021, ambao ni wa muhimu katika Mkakati wa Kukua kwa Uchumi ha Kupunguza Umasikini (NSGRP/MKUKUTA II, 2010-2016). Licha ya juhud zote za kitaifa, taifa bado linakabiliana na maadui wale wale wakubwa watatu, umasikini, maradhi na ujinga.

Katika kujaribu kujazia maarifa kuhusu pengo la umasikini, matokeo yanayotokana na utafiti huu yaliyowasilishwa katika ripoti hii yalipelekea Timu ya ATD ya mradi wa Utafiti kufikia katika maamuzi kwamba:

Kwanza, umasikini unaathiri idadi kubwa ya wananchi wa kawaida ndani na nje ya Tanzania. Kulingana na kipimo cha (HBS1) kilicho katika msingi wa kielelezo cha ulaji wakila mtu ambacho kinapima uwiano wa idadi ya watu na kiwango cha ulaji chini ya mstari wa 2 wa umasikini. Juhudi zozote katika kuelezea tatizo zitahitaji kuwashisha wahanga hawa wa umasikini katika michakato ya kutengeneza sera pia katika tafiti ili kuweza kubadilisha namna umasikini na watu wanaouishi wanavyotendewa. Kazi ya utafiti katika taarifa hii imewe ka wazi maarifa tele na utambuzi wa uwezo wa watu ambao kawaida hawasikiki ambao kwa kawaida wanaishi katika umasikini uliokithiri katika maeneo yaliyokuwa yamechaguliwa kufanya utafiti huu.

Pili, kila binadamu ana haki ya kuheshimiwa na kutambuliwa. Hizi ni silaha za muhimu katika mapambano dhidi ya janga la umasikini mionganoni mwa wananchi wa kawaida.

Watunga sera, wanataaluma, watangazaji wa habari na wanateknokrasia wanatakiwa kuelewa kwamba bila kuwashemu na kuwashisha watu wanaoishi katika umasikini, hakutakuwepo na maana ya maendeleo ya uchumi jamii na mapambano dhidi ya umasikini yataendelea kuwa magumu kama siyo kushindikana kabisa.

Kwa mtazamo huo, Timu ya ATD ya mradi wa Utafiti inatoa baadhi ya mapendelekezo muhimu ya sera kama ifuatavyo:

- 1.** Timu ya ATD ya mradi wa Utafiti inapendekeza kwamba uhakiki wa sera za umma yafanyike kuhakikisha kwamba vipimo vipyta vya umasikini vilivyoibuliwa katika utafiti huu ukiacha kipimo cha Umasikini wa Kipato vipewe umuhimu ili kuboresha sera zilizopo na mifumo ya taasisi zetu.
- 2.** Ili kuweza kuelezea mapungufu katika utekelezaji wa sera za taasisi Timu ya ATD ya mradi wa Utafiti inapendekeza utekelezji imara wa mfumo wa uratibu wa kitaifa wa sera za maeneo katika kuhamasisha uchumi - jamii ulio na tija. Hii inawezekana kwa kuwahusisha wadau wote kama vile washirika wa maendeleo, vyama vya kijamii, mashirika yenye asili ya kiimani, na sekta binafsi inayosisimka kupitia “public – private partnership” (PPP), pamoja na watu wanaoishi katika umaskini uliokithiri na wengineo.¹
- 3.** Timu ya ATD ya mradi wa Utafiti inapendekeza kuhamasisha juhudhi za makusudi katika sera zinazolenga pamoja na mengine, kuondoa umasikini na kuboresha maisha ya watu, kujenga uwezo wa jumuiya maskini na kuelimisha umma kwa ujumla kuhusiana na heshima na utu wa watu wanaoishi katika umasikini uliokithiri. Zaidi ya hayo, mabadiliko yanapaswa yafanyike katika sera za maeneo kama vile kilimo, jinsia, masuala ya watoto, sheria za ndoa, na sekta isiyo rasmi ambayo ni chanzo kikuu cha pato kwa watu wanaoishi katika umasikini uliokithiri.
- 4.** Timu ya ATD ya Mradi wa Utafiti inapendekeza mfumo imara wa kisheria utakaosaidia sera hizo hapo juu kuwafaidisha watu masikini. Uzoefu unaonesha kwamba Tanzania inazo sera nzuri sana lakini bila utekelezaji wa kisheria zinakuwa vigumu kutekelezeka. Kwa kuongeza, watu wanaoishi katika umaskini uliokithiri ni ushahidi hai wa ukiukwaji wa haki za binadamu. Umasikini ni ukiukwaji wa haki za binadamu kwa namna unavyo sababisha maumivu kwa wahanga wake, hivyo mifumo ya Tanzania ya sheria na sera lazima iwekee maanani suala kwamba umasikini uliokithiri ni uvunjaji wa haki za binadamu na hivyo lazima utokomezwe.
- 5.** Timu ya utafiti ya ATD inapendekeza kwamba sera za kitaifa zitilie maanani tofauti na mifanano ya watu wanaoishi katika umasikini maeneo ya mijini na vijijini kwa kuwa wanataka mifumo inayostahili ya kisheria na kitaasisi kama inavyoainishwa katika taarifa hii.
- 6.** Timu ya ATD ya Mradi wa Utafiti inapendekeza kwamba taasisi za kitaifa na vituo vya utafiti vitumie mbinu ya Uunganishaji Maarifa kama namna mpya ya utafiti shirikishi. Hii itasaidi kuongeza siyo tu uzalishaji wa maarifa lakini pia ushiriki halisi wa watu wanaoishi katika umasikini uliokithiri kama watafiti wenza na waibuaji wenza wa maarifa.

¹ Household Baseline Survey, 2011/12, p.7


² 28.2 % ya Watanzanian hawawezi kufikia mahitaji yao ya msingi ya uhitaji wa ulaji na 9.7 % ya idadi ya watu wanaoishi katika umasikini uliokithiri hawana uwezo wa kununua chakula cha walao kuweza kufikia mahitaji yao ya chini ya lishe ya (Kcal) 2,200 kwa mtu mzima kwa siku.

Matokeo ya uunganishi wa utafiti wa Kimataifa wa “Vipimo vya Umaskini Vilivyojificha”.

Utafiti ulihuisha timu za Bangladesh, Bolivia, Ufaransa, Tanzania, Uingereza na Marekani.

Watu walio na uzoefu wa moja kwa moja na umaskini, wataalamu na wanataluma walifanya kazi pamoja bila ubaguzi.

Utafiti unajulikana kwa jina la “Uunganishaji wa Maarifa”



- **UZOEFU WA MSINGI**
- **MAHUSIANO YANAYOBADILIKI**

- **MAHUSIANO BINAFSI**
- **SABABU ZINAZOBORESHA**

Timu ya utafiti ya ATD Tanzania



Prof. KITOJO WETENGERE



GABRIEL CHACHA SASI



PELAGIE MUKAMPAMIRA



ALEXIE GASENGAYIRE



SALEHE MUSSA SEIF



FRATELINE KASHAGA



CONSTANTINE SAASITA MUNEMA



ABDALLAH H. JUMA



UPENDO SPORA CHRISTOPHER



ELIMINA JOHN FUNGA



REHEMA JACKSON MAPUNDA



KASIANI HILALI RAMADHANI



ASHA ATHUMANI MOHAMED



YUSUFU HAMISI MKUTI



VENANCE FRANCIS

MBERA

Kiambatanisho 1

Idadi ya vikundi rika vya watu wanaoishi katika umaskini vilivyofikiwa katika maeneo yaliyokuwa yamechaguliwa kwa utafiti.

Mkoa	Wilaya	Kijiji/Mtaa	Aina ya kikundi rika	Idadi ya vikundi	Idadi ya washiriki	
					Ke	Me
Dar es Salaam	Manispaa ya Kinondoni	Tegeta/ Kunduchi mtongani	Wanaume watu wazima	1		6
			Wanawake watu wazima		7	
			Wanaume wazee	1		6
			Vijana	1	4	4
		Boko	Watoto miaka 16	1	2	5
			Wanawake watu wazima	1	7	
			Wanaume watu wazima	1		6
		Pakacha/ Tandale	Walemavu	1	5	2
			Wanawake wazee	1	7	
			Watoto < miaka 16	1	4	4
			Wadada poa	1	7	
		Kambangwa	Wanaume watu wazima (NRT)	1	3	3
		Manispaa ya Ilala	Kwabukuru/ Kipawa mji mpya	Wanaume watu wazima	1	6
				Wanawake watu wazima	1	6
				Wazee	1	6
			Kivukoni (Ferry)	Wanawake watu wazima	1	7
				Wanaume watu wazima	1	7
Dodoma	Kondo: Vijijini	Keikei na sambwa	Watu wazima	1		7
			Watu wazima	1	7	
	Bahi: Vijijini	Igubule na Khome	Watu wazima	1		7
			Watu wazima	1	7	

Mkoa	Wilaya	Kijiji/Mtaa	Aina ya kikundi rika	Idadi ya vikundi	Idadi ya wasini iki	
					Ke	Me
Kigoma	Kigoma Ujiji: mjini	Rubuga P/School	Watoto <miaka16	1	4	4
		Kibirizi P/School	Watoto<miaka16	1	4	3
	Kibondo: Vijijiini	Lusohoko P/school	Watoto <miaka16	1	4	4
		Kibondo P/School	Watoto<miaka16	1	3	4
Kilimanjaro	Moshi: Mjini	Mwereni P/School	Watoto <miaka16	1	4	4
	Hai vijijiini	Mkarama P/school	Watoto <miaka16	1		4
Njombe	Njombe Mjini	Idundilanga & Kambarage	Wanaume wazee	1	5	
			Wanawake wazee	1	7	
	Ludewa Vijijiini	Luvuyo & Mangalanyene	Wanaume wazee	1		7
			Wanawake wazee	1	6	
Jumla				34	110	106

Kiambatanisho 2

Idadi ya vikundi-rika vya watu wasioishi katika umaskini yaani wataalamu na wanataaluma waliofikiwa katika maeneo yaliyochanguliwa kwa ajili utafiti.

Mkoa	Wilaya	Taasisi	Aina ya kikundi rika	Idadi ya vikundi	Idadi ya washiriki	
					Ke	Me
Dar es Salaam		Mwalimu Nyerere Memorial Academy Tanzania	Wanataaluma	1	4	2
		-Mozambique Center for Foreign Relations	Wanataaluma	1	4	2
	Kinondoni Kunduchi	Mbalimbali	Wataalamu	1	3	3
	Kambangwa	Mbalimbali	Wataalamu	1	2	1
	Ilala	Mbalimbali	Wataalamu	1	3	3
Dodoma	Dodoma mjini	Dodoma Rural Planning Development College	Wanataaluma	1	5	1
	Kondo (Keikei)	Mbalimbali	Mbalimbali	1	3	4
	Bahi (Nk'home)	Mbalimbali	Wataalamu	1	4	3
Njombe	Njombe mjini	Tumaini Business Management College and Njombe Focal Development College	Wanataaluma	1	5	2
		Mbalimbali	Wataalamu	1	3	4
		Mbalimbali	Wataalamu	1	5	1
Jumla				11	41	26

Kiambatanisho 3

VIPIMO VYA UMASKINI, WANAUUME NA WANAWAKE KUTOKA VIJIJINI NA MIJINI.

Wanawake Vijijini	Wanaume Vijijini	Wanawake Mijini	Wanaume Mijini
<p>1. Njaa ya kila mara</p> <p>2. Mbinu Duni za Kilimo</p> <p>3. Afya Duni</p> <p>4. Ukosefu wa huduma za ushauri</p> <p>5. Umaskini wa ukoo</p> <p>6. Elimu Duni</p> <p>7. Vurugu katika familia</p> <p>8. Unyonyaji wa Kiuchumi</p> <p>9. Ukosefu wa maji</p> <p>10. Kukosa mshikamano, ushirikiano na kusaidiana katika jamii</p> <p>11. Ukosefu wa usawa wa kijinsia</p> <p>12. Ndoa za utotonii</p> <p>13. Huduma za afya ziko mbali</p> <p>14. Ushirikiano wa watu wanaoishi katika umaskini</p>	<p>1. Mbinu duni za kilimo</p> <p>2. Ukosefu wa Uongozi bora</p> <p>3. Kukosa ujuzi wa ujasiriamali</p> <p>4. Umaskini mkali</p> <p>5. Kukosa Huduma za Ushauri</p> <p>6. Mmomonyoko wa Maadili</p>	<p>1. Makazi duni</p> <p>2. Uvivu</p> <p>3. Sera, Mbovu za Jamii</p> <p>4. Ukosefu wa usalama</p> <p>5. Mfumo Dume</p> <p>6. Elimu Duni</p> <p>7. Umaskini wa Kipato</p> <p>8. Imani za uchawi na ushirikina</p> <p>9. Ukosefu wa amani</p> <p>10. Unyonyaji wa maskini</p> <p>11. Kutengwa na jamii</p> <p>12. Ukatili wa Kijinsia</p> <p>13. Rushwa</p> <p>14. Chuki na vivu</p> <p>15. Desturi na kanuni potoshaji</p> <p>16. Migongano katika Familia</p> <p>17. Maisha ya tabu</p> <p>18. Hali ya Kutokujtambua</p> <p>19. Ukosefu wa viwanda</p> <p>20. Madhara ya Kisaikolojia yanayosababishwa na Umaskini</p> <p>21. Kutengwa</p> <p>22. Uvivu</p>	<p>1. Umaskini wa Kipato</p> <p>2. Udhaliilishwaji</p> <p>3. Vurugu</p> <p>4. Ukandamizaji</p> <p>5. Elimu Duni</p> <p>6. Kuporomoka Maadili</p> <p>7. Upweke</p> <p>8. Athari za Kisaikolojia</p> <p>9. Afya Duni</p> <p>10. Haki za Binadamu</p> <p>11. Tabia</p>

Kiambatanisho 4

VIPIMO VYA UMASKINI VYA WATU WANAOISHI KATIKA UMASKINI KUTOKA MAENEYO YA MIJINI NA VIJIJINI

Vipimo vya watu wanaoishi katika umaskini kutoka maeneo ya vijijini	Vipimo vya watu wanaoishi katika Umaskini kutoka maeneo ya mijini
<ol style="list-style-type: none">1. Kukosa usalama2. Matarajio hafifu katika maisha3. Unyanyasaji na unyonyaji wa watoto4. Unyonyaji wa uchumi wa kijamii5. Ushiriki hafifu6. Huduma hafifu za Afya7. Umaskini wa Kipato8. Ukosefu wa maji safi9. Uonevu kwa wanawake10. Elimu Duni11. Changamoto na vikwazo wanavyokabiliana navyo wakulima wadogo wadogo12. Uongozi na Utawala mbovu13. Uharibifu wa Mazingira14. Mmomonyoko wa maadili katika jamii	<ol style="list-style-type: none">1. Umaskini wa Kipato2. Afya mbovu3. Athari za Kisaikolojia zinazotokana na Umaskini4. Tabia mbaya katika jamii5. Ukosefu wa Elimu6. Uvunjifu wa Haki za Binadamu7. Imani Potofu8. Kufanya kazi na kuishi katika hali isiyo salama9. Kuishi katika mazingira duni10. Kutengwa na jamii11. Matarajio hafifu katika maisha12. Sera mbovu kwa watu wanaoishi katika umaskini.

Kiambatanisho 5

KIKUNDI RIKA CHA VIJANA KATI YA MIKA 16 NA 18

KIKUNDI RIKA CHA WALEMAVU WA VIUNGO	WADADA POA	KIKUNDI RIKA CHA VIJANA KATI YA MIKA 16 NA 18 16 AND 18 AGE
1. Unyanyasaji 2. Afya mbovu 3. Upweke 4. Kipato duni 5. Unyanyapaa	1. Elimu Duni 2. Mila na Desturi 3. Kipato Duni 4. Kuvunjika kwa ndoa 5. Kutokujua sheria 6. Tabia	1. Maadili mabovu 2. Kutokuheshimiwa 3. Kipato Duni 4. Upweke

Kiambatanisho 6

ORODHA YA VIPIMO VYA UMASKINI KUTOKA KWA WANAWAKE WAZEE VIJJINI NA MIJINI.

Vikundi rika vya wanawake wazee kutoka vijijini	Vikundi rika vya wanawake wazee kutoka mijini
1. Upweke 2. Elimu Duni 3. Umaskini wa Kipato 4. Uonevu wa wanawake 5. Uonevu na kunyimwa haki wanawake 6. Kutumia maarifa na juhudzi zako mwenyewe 7. Utengemezi katika kanuni za kimila katika utatuzi wa matatizo 8. Unyonyaji wa watu wanaoishi katika umaskini	1. Kipato Duni 2. Uvumilivu 3. Elimu Duni 4. Athari za kisaikolojoa zinazotokana na umaskini uliokithiri 5. Kutengwa 6. Uonevu wa wanawake 7. Kujutia maisha ya umaskini 8. Kutumia mbinu za kienyeji kukabiliana na changamoto za umaskini 9. Uvumilivu dhidi ya mateso

Kiambatanisho 7

ORODHA YA VIPIMO VYA UMASKINI VYA WAZEE WANAUUME KUTOKA VIJIJINI NA MIJINI

VIKUNDI RIKA VYA WAZEE KUTOKA MIJINI	VIKUNDI RIKA VYA WAZEE KUTOKA VIJIJINI
<ol style="list-style-type: none">1. Uvivu2. Kunyanyapaliwa3. Kukabiliwa na Umaskini4. Kukosa Elimu iliyo rasmi5. Vurugu6. Huduma duni za Afya7. Upweke8. Kipato Duni9. Miundombinu mbovu	<ol style="list-style-type: none">1. Athari za kisaikolojia zinazotokana na umaskini2. Umaskini wa Kipato3. Utawala mbovu4. Mmomonyoko wa maadili

Kiambatanisho 8

ORODHA YA VIPIMO VYA UMASKINI WATAALAMU KUTOKA MIJINI NA VIJIJINI

VIKUNDI RIKA VYA WATAALAMU KUTOKA MIJINI	VIKUNDI RIKA VYA WATAALAMU KUTOKA VIJIJINI
<ol style="list-style-type: none">1. Haki za binadamu2. Afya mbovu3. Elimu Duni4. Tabia5. Uchumi Duni6. Kipato Duni7. Utunzaji mbovu wa rasilimali8. Uharibifu wa mazingira9. Athari za Kisaikolojia10. Mazingira mabovu11. Ushiriki hafifu12. Mila na tamaduni potoshaji13. Matatizo ya Kisaikolojia	<ol style="list-style-type: none">1. Elimu Duni2. Kutokujitambua3. Kutokuwajibika4. Kukosa utu5. Mazingira Duni6. Kipato Duni7. Huduma za Afya zisizoridhisha8. Uchumi Dhaifu9. Kukosa Ushirikiano10. Kutokuwa na kazi11. Ufahamu mdogo wa masuala ya Afya12. Uharibifu wa mazingira

Kiambatanisho 9

ORODHA YA VIPIMO VYA UMASKINI KUTOKA KWA WANATAALUMA

Vipimo kutoka kwa wanataaluma

1. Sababu za Kiuchumi
2. Sababu za Kijamii
3. Sababu za Kisiasa
4. Sababu za Mazingira na Makazi
5. Sababu za Tabia
6. Umaskini wa Kipato
7. Sababu za Kimazingira
8. Ushiriki mbovu
9. Huduma duni za Kijamii
10. Kutokuwepo utulivu katika jamii
11. Uongozi mbovu
12. Mtazamo hasi
13. Maarifa Duni au Elimu
14. Mtazamo au fikra hasi
15. Kukosa vipaumbele katika maisha
16. Umaskini wa raslimali
17. Afya mbovu
18. Sababu za Kidemografía

Kiambatanisho 10

**ORODHA YA VIPIMO VYA UMASKINI KUTOKA VIKUNDI RIKA VYA WATOTO
KATI YA UMRI WA 9-14 KUTOKA MIJINI NA VIJJINI.**

VIKUNDI VYA MJINI	VIKUNDI VYA VIJJINI
<ol style="list-style-type: none">1. Ukatili dhidi ya watoto2. Watoto wa mitaani3. Hali duni ya maisha4. Umaskini wa Kipato na mtaji5. Huduma duni za wazazi6. Maisha duni7. Watoto kulazimishwa kufanya kazi8. Elimu Duni	<ol style="list-style-type: none">1. Mateso na maisha magumu kwa watoto2. Kukosa mahitaji ya watoto3. Matatizo ya Umaskini unaohusiana na makazi4. Kutokuheshimika5. Umaskini wa Kipato6. Huduma Duni za Afya7. Kukosa furaha kwa kutokusikika8. Ulinzi na mwongozo mdogo kutoka kwa wazazi9. Ujasiri na mshikamano wa watoto shulenii10. Maisha ya hali ya chini11. Athari za Kisaikolojia zinazotokana na umaskini12. Mazingira duni ya makazi13. Kubaguliwa



ATD Fourth World Tanzania
Kinondoni District, Mwananyamala,
Kambangwa, Igusure Street.
P.O Box 61786
www.atd-fourthworld.org

Phone: +255 (0) 717 413 414
Email: national.team.tanzania@atd-fourthworld.org



@ ATD Tanzania